

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



29 OKTOBA, 2021

TAARIFA KWA UMMA

ZIARA YA MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mh. Amos Makalla leo amefanya ziara katika Wilaya ya Kinondoni kukagua miradi mitatu ya Ujenzi wa Jengo la Utawala, Uwanja wa Mpira wa Miguu na standi ya Mabasi mwenge ambayo utekelezaji wake ulisimamishwa kwa muda na waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mh. Umy Mwalimu ilikupisha uchunguzi kujua sababu zilizo sababisha kutoa kamilika kwa wakati.

Akizungumzia malengo ya ziara hiyo alisema "Alipewa kazi na Waziri Ofisi Rais, Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mh. Umy Mwalimu kuitembelea miradi hii ilikuona hatua ya utekelezaji na dosari zilizopo na kujiridhisha kabla ya kutoa kibali cha maandishi kuruhusu kuendeleza utekelezaji wake".

Akihitimisha ziara yake. Mh. Mkuu wa Mkoa aliwapongeza Viongozi na Watendaji wote wa Kinondoni kwa kubuni miradi mikubwa ya kuongeza mapato ya Halmashauri na Serikali kuu inayotekelezwa kwa mapato ya ndani kwa mtindo wa "force Account" hivyo akatoa rai kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kwa kuelekeza nguvu katika miradi Michache yaani ya Uwanja wa Mpira wa Miguu na Standi ya Mwenge ili kuwezesha kukamilika kwa wakati badala ya kutekeleza miradi mingi kwa wakati mmoja na hivyo kuifanya kuwa na dosari ya kusuasua katika ukamilishaji wake.

Mh. Makalla amesema, "hakuona dosari inayohusiana na wizi wa fedha za Miradi isipokuwa changamoto na Dosari mbalimbali zilizopelekea miradi hiyo kusuasua kukamilika kwake kwa wakati na hivyo kumlazimu Mh. Waziri kuisimamisha kwa muda ili kutoa mwongozo na maelekezo ya namna bora ya kuitekeleza.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mh. Godwin Gondwe amemshukuru Mkuu wa Mkoa na kuahidi kutoa ushirikaiano mkubwa katika usimamizi wake mara kibali kitakapotolewa kwa kuondoa dosari zote zilizofanya Miradi hiyo kushindwa kukamilika kwa wakati.

Akizungumza kwa niaba ya Manispaa ya Kinondoni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Mh. Songoro Mnyonge alimshukuru Mkuu wa Mkoa na kumhakikishia kuwa Manispaa yake itazingatia maelekezo yote ikiwemo ushauri uliotolewa wa kuweka taa na eneo la kupaki magari katika uwanja wa mpira Mwenge ili uendane na hadhi yake.

Imetolewa na:-

Sebastan M. Mhowera

AFISA UHUSIANO
MANISPAA YA KINONDONI